

TAARIFA YA UTENDAJI WA SHIRIKA LISILOKUWA LA KISERIKALI (EMEDO)

Mwaka 2021 EMEDO ilitekeleza mraadi wa utafiti katika mikoa mitatu ambayo ni Mwanza, Kagera na Mara. Kwa upande wa wa Mwanza mradi huo ulifanyika wilaya za Nyamagana na Ukererwe, kwa upande wa wilaya ya Ukerewe utafiti ulifanyika vijiji vya Irondo na Musozi. UTAFITI huo ulikuwa juu ya Mitizamo ya hatari ya kuzama maji maeneo ya Ziwa Viktoria -maeneo yaliyoangaziwa ilikuwa ni - Kwanini ajali za kuzama wavuvi zinatokea, yapi matokeo ya kiuchuni na kijamii yanayosababishwa na vifo vya wavuvi hasa wanaotegemewa na familia zao, -Mitizamo ya jamii juu ya kuzama maji. Makundi yaliyohusishwa katika ukusanyaji wa taarifa za kitafiti ni wavuvi, wamiliki wa vyombo vya uvuvi, mafundi wa mitumbwi, BMU viongozi, wachakataji wa samaki, viongozi wa vijiji, wataalamu wilaya (Afisa maendeleo na adifa uvuvi



Picha ya pamoja Mgeni Kaimu katibu Tawala wilaya ya ukerewe pamoja na washiriki wa kikao .

Ukusanyaji wa taarifa ulifanikiwa kati ya mwezi wa tano na mwezi wa sita ukienda sambamba na mikutano ya jamii husika kwenye kila kijiji na wilayani ikilenga kutoa uelewa juu ya utafiti huo. EMEDO pia ilirejea mwezi wa tisa na kufanya mikutano na wataalamu wilayani na wanakijiji katika maeneo yao ikiwapa mrejesho uliotokana na utafiti uliofanyika. Lakini pia kupata maoni yao juu ya shughuli pendekezwa katika kushughulika na changamoto zilizoonekana kwenye utafiti.



Uwasilishaji wa mada ukiendelea katika ukumbi wa Monarch jana tarehe 5.09.2022

